# KUTATHMINI ATHARI ZA LUGHA YA KISUKUMA KATIKAKUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU

**PASCHAL MULIKUZA**

**TASNIFU HII IMEWASILILISHA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIACHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma na anapendekeza Tasnifuhii inayohusu ***Athari za lugha ya Kisukuma katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili Sanifu,*** ipokelewe na ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa ajili ya kukamilisha matakwa ya kuhitimu shahada ya uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.



……………………………………

Dkt. Salma Omar Hamad

(Msimamizi)

Tarehe ……………………………….

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi Paschal Mulikuza, ninatamka na ninathibitisha kwamba, Tasnifu hii iitwayo **Athari ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahli sanifu** ni kazi yangu mimi mwenyewe kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

………………………………..

Paschal Mulikuza

Tarehe ………………………….

## HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya Tasnifu hii hairusiwi kukaririwa, kunakiliwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote ile au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile au kurudufu katika hali yoyote bila kupata idhini ya mwandishi wa Tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa baba Martin Mulikuza na mama yangu Ephrata Martin kwa kunisomesha toka darasa la kwanza hadi Chuo Kikuu. Walinilea kwa kunitia moyo na kunihimiza kusoma kwa bidii, wamenipa msingi wa maisha katika dunia hii. Pia, bila kuwasahau ndugu zangu wapendwa, Jacob Mulikuza, Magreth Mulikuza, Noela Mulikuza pamoja na mtoto wangu Paschaline. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenisaidia na amenibariki katika kufanikisha kazi hii. Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Salma Omar Hamad kwa kubeba jukumu la kuisimamia vyema kazi hii. Nimemshukuru kwa ujasiri na uvumilivu wake mkubwa tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Ninaamini kuwa amenivumilia vya kutosha kwa udhaifu wangu kama binadamu na kama mwanafunzi. Mafanikio ya tasnifu hii yametokana na juhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa katika utafiti huu. Licha ya majukumu mengi aliyonayo hakusita hata mara moja kusoma kazi yangu kwa umakini mkubwa kwa wakati na kutoa maelekezo yanayojenga kazi hii kwa muda wote na wakati unaofaa. Sina cha kumlipa ila nina muombea dua kwa Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na amzidishie nguvu na imani ili aweze kutoa mchango kwa wanataaluma na taifa kwa ujumla. Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mchango wao walionipatia katika masomo yangu:

Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Nasra Habibu na mwalimu Bakari Kombo. Mungu awape maisha marefu na ya furaha katika maisha yao yote ili waendelee kutoa mchango wa kitaaluma na wa kijamii katika taifa letu. Vilevile ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya Uzamili ya Kiswahili wa mwaka wa masomo 2018/2019. Shukurani hizi za pekee zimetokana

na ushirikiano wao wa dhati kwa kipindi chote cha masomo ya uzamili. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa kupendana na kusaidiana. Vilevile, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wazazi wangu, Matrin Mulikuza na Ephrata Martin pamoja na familia yangu kwa kuniendeleza kielimu hadi kufikia hatua hii ya juu. Pia bila kuwasahau rafiki zangu Regina Cyrilo, David Mboya na Flora Kinyashi kwa msaada wao wa hali na mali. Mwenyezi Mungu awajalie afya tele na rehema tele.

## IKISIRI

Lengo la tasnifu ni kutathmini athari za lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi, sababu za athari hizo na mbinu za kutatua athari hizo. Utafiti huu umefanywa katika mkoa wa Tabora, wilaya ya Tabora mjini katika Shule za msingi za Mwenge, Isike, Mihayo na Kitete. Utafiti huu umetumia nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ambayo hutoa maelezo juu ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ambapo kwa muktadha wa kazi hii ni lugha ya Kisukuma na Kiswahili. Utafiti huu ulitumia mbinu mbili za ukusanyaji data ambazo ni; hojaji na mahojiano. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu yenye madhumuni maalumu na mbinu bahatishi. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa, athari za matamshi zinazojitokeza kwa wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Athari hizo ni pamoja na udondoshaji wa sauti, kutumia sauti zinazokaribiana, athari za kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu. Data za utafiti huu zinathibitisha kuwa kuna athari za kimofolojia za lugha ya kisukuma ambazo pia zinajitokeza kwa wazungumzaji wa kisukuma wanaojifunza Kiswahili sanifu. Miongoni mwa athari zilizobainika ni kuongeza viambishi visivyohitajika katika maneno. Kiwango cha athari za kifonolojia na kimofolojia alizogundua mtafiti, ilihusisha matamshi, kuongeza viambishi ambavyo vilitokana katika lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumiwa na Taasisi ya ukuzaji mitaala kutoa mapendekezo kwa wanaojifunza Kiswahili kwa kuwashirikisha wanafunzi kimazungumzo kwa lengo la kuinua kiwango cha umilisi wa lugha. Hitimisho kwanza utafiti huu umeshughulikia athari za Lugha ya Kisukuma katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu, ni matarajio ya mtafiti kwamba, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti juu ya athari za lugha nyingine za Kibantu zinazotokana na tofauti za kisarufi baina ya lugha hizi mbili.

# YALIOMO

UTHIBITISHO ..... ii

TAMKO LA MTAHINIWA ..... iii

HAKI MILIKI ..... iv

TABARUKU ..... v

SHUKURANI ..... vi

IKISIRI ..... viii

YALIOMO ..... ix

ORODHA YA MAJEDWALI ..... xiii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1**

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 1

1.2 Tatizo la Utafiti ..... 4

1.3 Malengo ya utafiti ..... 4

1.3.1 Lengo kuu ..... 4

1.3.2 Malengo mahususi ..... 4

1.4 Maswali ya Utafiti ..... 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 5

1.6 Mipaka ya Utafiti ..... 6

1.7 Mpangilio wa Tasnifu ..... 6

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ..... 7**

2.1 Utangulizi ..... 7

2.2 Fasili ya Dhana ya Sarufi ..... 7

2.2.1 Fasili ya dhana ya Fonolojia ........................................................................ 7

2.2.2 Fasili ya dhana ya Fonimu ........................................................................... 8

2.2.3 Fasili ya dhana ya Mofolojia ......................................................................... 9

2.2.4 Fasili ya dhana ya mofimu ............................................................................ 9

2.2.5 Fonolojia ya Kiswahili .................................................................................. 10

2.2.5.1 Fonimu za irabu/vokali za Kiswahili sanifu ............................................. 10

2.2.5.2 Viyeyusho/fonimu za nusu irabu za Kiswahili sanifu ............................... 11

2.2.5.3 Fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu ............................................... 12

2.2.5.4 Miundo ya silabi katika lugha ya Kiswahili ............................................. 14

2.2.6 Fonolojia ya kisukuma .................................................................................. 17

2.2.6.1 Dhana ya Irabu katika lugha ya Kisukuma ............................................... 17

2.2.6.2 Dhana ya konsonanti katika lugha ya Kisukuma ...................................... 20

2.2.6.3 Miundo ya silabi katika lugha ya Kisukuma ............................................. 22

2.2.6.4 Athari ya lugha za Kibantu katika lugha ya Kiswahili .............................. 24

2.2.7 Kiunzi cha nadharia ....................................................................................... 25

2.3 Muhtasari ........................................................................................................ 29

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................................... 30**

3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 30

3.2 Mkabala wa Utafiti .......................................................................................... 30

3.3 Eneo la utafiti .................................................................................................. 30

3.4 Sampuli na Usampulishaji ............................................................................... 31

3.5 Ukusanyaji wa Data ........................................................................................ 34

3.5.1 Mbinu za kukusanyia Data ............................................................................ 34

3.5.1.1 Mahojiano ........ 35

3.5.1.2 Mbinu ya hojaji ........ 35

3.6 Uchanganuzi wa Data ........ 36

3.7 Maadili ya Utafiti ........ 37

3.8 Hitimisho ........ 37

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI DATA ........ 38**

4.1 Utangulizi ........ 38

4.2 Athari za Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili Sanifu ........ 38

4.2.1 Athari za Kifonolojia ........ 39

4.2.2 Athari za matumizi ya /l/ badala ya /r/ ........ 39

4.2.3 Athari za matumizi ya /bh/ ........ 41

4.2.4 Athari katika matumizi ya / ð / ........ 42

4.2.5 Athari katika matumizi ya / γ / ........ 43

4.2.6 Athari katika matumizi ya / Ɵ / ........ 44

4.3 Athari za Kimofolojia ........ 46

4.3.1 Matumizi ya kiambishi ‘ga’ ........ 47

4.3.2 Matumizi ya kiambishi ‘gi’ ........ 48

4.4 Viwango vya utokeaji wa athari za kifonolojia, na kimofolojia za lugha yaKisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu ........ 50

4.5 Hitimisho ........ 54

**SURA YA TANO: HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO ........ 55**

5.1 Utangulizi ........ 55

5.2 Muhtasari kwa ujumla wa Utafiti ................................................ 55

5.3 Muhtasari wa matokeo ................................................ 56

5.4 Hitimisho ................................................ 56

5.5 Mapendekezo ya Utafiti ................................................ 57

**MAREJELEO ................................................ 58**

**VIAMBATANISHO ................................................ 62**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 2.1 Vitamkwa konsonanti vya kiswahili ........................................... 13

Jedwali Na. 2.2 Konsonanti zipatikanazo katika lugha ya kisukuma .................... 21

Jedwali Na. 3.1 Mgawanyo wa Sampuli............................................................... 33

Jedwali Na. 4.1 Athari za Kifonolojia Katika Matamshi kwa Wanafunzi wa shule za msingi ...................................................................... 42

Jedwali Na 4.2 Athari za Kifonolojia Katika Matamshi kwa wazee wa Kisukuma ......................................................................... 46

Jedwali Na. 4.3 Jedwali la watafitiwa walimu linalo onesha idadi na majibu yao. ....................................................................................... 48

Jedwali Na. 4.4 La watafitiwa linalo onesha idadi ya kiwango cha athari za kifonolojia katika Kiswahili sanifu. ............................................ 52

Jedwali Na 4.5 La watatitiwa i linalo onesha idadi ya kiwango cha athari za kimofolojia katika Kiswahili sanifu ............................................ 53

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tanzania ni nchi yenye makabila 125 hali inayosababisha kuwa na lugha za makabila 125 Muungwana blog (2017). Stern (1983) anaeleza kwamba lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtoto huipata kutoka kwa mama yake mzazi angali mchanga. UNESCO (2003) wanaeleza kwamba lugha ya kwanza ni ile lugha ambayo mjifunzaji anajifunza kwanza kabla ya lugha nyingine ambayo inajulikana kama lugha mama ya mjifunzaji Hata hivyo, licha ya Watanzania kuwa na lugha zao za makabila zikiwa ndizo lugha mama, Pamoja na hayo, kinadharia ujifunzaji wa lugha ya kwanza unahusisha kipindi maalumu ambapo kipindi hicho kikipita mjifunzaji anakuwa hana uwezo wa kuimudu lugha hiyo vizuri. Kwa mujibu wa nadharia tete ya kipindi faafu ya Lenneberg (1967) ujifunzaji wa lugha ya kwanza unakoma baada ya baleghe. Hii ina maana kwamba kama mtoto anakuwa hajaimudu vizuri lugha anayojifunza mpaka kipindi cha baleghe ni vigumu kupata umilisi wa lugha hiyo baada ya hapo. Hata hivyo, kwa mujibu wa Jackendoff (1994) watoto wanaweza kuujenga mfumo changamani wa lugha wanayojifunza katika muda wa miaka miwili mpaka mitano. Kwa mfano mtoto wa miaka mitatu ana uwezo wa kuunda na kuelewa sentensi changamani ya lugha ya kwanza yao bila muongozo wa moja kwa moja kutoka kwa walezi (O’Grady; 2008). Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba mjifunzaji wa lugha ya kwanza anapofikia umri wa baleghe anakuwa tayari ameshaimudu mifumo yote ya lugha yake ya kwanza.

Kwa upande mwingine lugha ya pili ni ile lugha ambayo mtu anajifunza baada ya ile lugha ya awali kuifahamu. Kwa mujibu wa Stern (1983) lugha ya pili ni ile lugha

ambayo mtu hujifunza mbali na lugha mama yake. Kwa mujibu wa Chaochuan (2005) ujifunzaji wa lugha ya pili unafanyika katika hali ya ung'amuzi tambuzi ambayo inatokea kwa watu wazima na watoto wajifunzao lugha wakiwa na malengo maalumu na mazingira mahususi kama vile darasa na mwalimu. Aidha, Saville-Troike (2006) amefasili dhana ya lugha ya pili kwa mapana zaidi, licha ya kukubali kwamba ni lugha ambayo huja baada ya kuwa mtu tayari ana lugha mama, yeye alienda mbali zaidi kwa kuhusisha lugha ya pili na nguvu, majukumu na dhima ya lugha hiyo katika jamii. Hivyo, anafasili lugha ya pili kuwa ni ile lugha rasmi au yenye kuhitajika kutumiwa katika masuala ya elimu, ajira na malengo mengine ya msingi kama ya kijamii (biashara, utalii na utambulisho). Kutokana na fasili hizi, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili kwa Wasukuma walio wengi hasa waishio vijijini kwani hujifunza na kuitumia lugha hii wakiwa tayari wana lugha yao ya Kisukuma ambayo wanaitumia katika maeneo wanayoishi. Lugha ya kwanza ni Kisukuma ambayo hujifunza na kuitumia katika mazingira ya nyumbani na wazazi wao mpaka muda wa kuanza shule za msingi. Pia, lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika elimu ya msingi na kama somo kwa shule za sekondari katika jamii pana ya Tanzania, Wasukuma wakiwa miongoni mwao.

Kwa asilimia kubwa Watanzania wanaunganishwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, kutokana na wazungumzaji hawa wanaozungumza lugha zao za Kibantu kuzungumza pia Kiswahili, Kiswahili kina mwingiliano mkubwa na lugha hizo za Kibantu. Masebo (2008:31-33) anaeleza kwamba lugha ya Kiswahili iliingiliana na lugha nyingine za Kibantu kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili katika jamii nyingi za Kibantu. Naye Mekacha (2011), anaeleza kwamba lugha moja huathiriwa

kutokana na muktadha wa matumizi yake. Anabainsha pia kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa hasa katika shughuli za kijamii zaidi kama vile shuleni, ofisini, sehemu za biashara na sehemu ambazo kuna makabila mengi. Watu wanapokuwa nyumbani kwao kwa asilimia kubwa hutumia lugha zao za asili. Kwa ujumla mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha kuathiriana kwa lugha hizo kwa sababu kila lugha huchukua baadhi ya misamiati kutoka katika lugha nyingine na kuuingiza katika lugha yake. Wazungumzaji wa lugha hizo wakizungumza kuna baadhi ya tofauti hutokea katika viwango mbalimbali vya kiisimu ikiwemo mofolojia, fonolojia, semantiki na sintaksia.

Tafiti mbalimbali zinazobainisha athari za lugha za kwanza kwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili zimeshafanyika. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa Nyanda (2015) ambaye amechunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili (ambapo katika utafiti wake ameonesha lugha ya kwanza ni kinywamwezi na lugha ya pili ni Kiswahili) na Wenceslaus (2015) aliyechunguza athari za lugha ya Kijita Katika kujifunza lugha ya Kiswahili (ambapo katika utafiti wake ameonesha lugha ya kwanza ni kijita na lugha ya pili ni Kiswahili). Kwa ujumla tafiti hizi zimeonesha athari za kifonolojia na za kimsamiati katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Pamoja na tafiti hizo ipo haja ya kiutafiti ya kutathmini athari ya lugha ya Kisukuma katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu ili kubaini ni athari zipi zinazotokana na mwingiliano wa Kisukuma na Kiswahili sanifu. Hivyo utafiti huu unalenga kufanya tathmini ya athari ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili ni athari ya lugha zao za kwanza, Tafiti mbalimbali zinazobainisha athari za lugha za kwanza kwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili zimeshafanyika. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa Nyanda (2015) ambaye amechunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili na Wenceslaus (2015) aliyechunguza athari za lugha ya Kijita Katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla tafiti hizi zimeonesha athari za kifonolojia na za kimsamiati katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kwa kuwa kila lugha ina muundo wake na tabia zake ni dhahiri kuwa athari za lugha ya kwanza kwa mjifunzaji wa lugha ya pili zina upekee pia. Aidha, tafiti zilizotangulia hazikugusia chochote kuhusu kiwango cha utokeaji wa athari hizo, yaani ni athari ipi inatawala zaidi wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Suala hili litafanyiwa kazi katika utafiti huu.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo ya aina mbili, nayo ni lengo kuu na malengo mahususi

### 1.3.1 Lengo kuu

Kutathmini athari za lugha za Kisukuma kama lugha ya kwanza katika kujifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili.

### 1.3.2 Malengo mahususi

1) Kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kisukuma kwa Wasukuma wanaojifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

2) Kuchunguza athari za kimofolojia za lugha ya Kisukuma kwa Wasukuma wanaojifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

3) Kubainisha kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia, na kimofolojia za lugha ya Kisukuma kwa Wasukuma wanaojifunza Kiswahili sanifu.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

1) Kuna athari gani za kifonolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

2) Kuna athari gani za kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

3) Kuna viwango vipi vya utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia za Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kufanyika kwa utafiti huu kutatoa mchango mkubwa wa kitaalamu, kitamaduni na kinadharia. Kwa upande wa taaluma, utafiti utapunguza pengo la kiutafiti juu ya athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili ambao kwa uelewa wa mtafiti, hakuna utafiti uliofanyika kwa kina juu ya mada hii. Hivyo utawasaidia wataalamu wa elimu kama vile waalimu na wanafunzi kutatua changamoto zitakazoweza kujitokeza wakati wa kujifunza na kufundisha lugha ya Kiswahili, walimu watabainisha umuhimu wa matamshi mazuri kwa wanafunzi ya lugha ya Kiswahili sanifu, wanafunzi watabaini umuhimu wa kutokuongeza viambishi visivyo hitajika kwa kuviamisha kutoka katika lugha mama ambayo ni kisukuma.

Aidha, kupitia utafiti huu jamii itakuwa na uelewa juu ya athari ya lugha Kisukuma kwa Wasukuma wanaojifunza lugha ya Kiswahili na hivyo kushirikiana na wadau wa

elimu katika kufanikisha suala la uzungumzaji lugha ya Kiswahili kwa usanifu; Vilevile Wizara ya Elimu na ufundi stadi ikishirikiana na waandaaji wa mitaala ya elimu wataweza kwa pamoja kusaidia katika kuhamasisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa usanifu zaidi na kuendeleza lugha hiyo. Pamoja na hayo, utafiti huu utakuwa kichocheo cha tafiti nyingine kuhusu kuathiriana kwa lugha ya kisukumana lugha ya Kiswahili na pia utaongezea marejeo.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili, ieleweke kuwa athari hizo ni zile zinazobainishwa na tofauti baina ya lugha ya Kisukuma na Kiswahili sanifu kama vile kimatamshi, kimsamiati na kimaana. Aidha utafiti huu ulihusisha wazee ambao ni wakabila la Kisukuma na wataalamu wa lugha ya Kiswahili.

## 1.7 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii imeundwa kwa jumla ya sura kuu tano ambapo sura ya kwanza ni utangulizi, ambao umewasilisha vipengele vyote muhimu vilivyoonesha haja ya kufanyika kwa utafiti huu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia na sura ya tatu ni mbinu za utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na sura ya tano inahusu hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali, kiunzi cha nadharia na pengo la utafiti. Kazi tangulizi zimegawanywa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza itatoa fasili ya dhana, sehemu ya pili itafafanua sarufi ya Kiswahili na sehemu ya tatu itafafanua sarufi ya Kisukuma.

## 2.2 Fasili ya Dhana ya Sarufi

Baada ya kusoma au kuishi na watu wa lugha hiyo. Kanuni, sheria au taratibu hizo hutawala kila moja kati ya viwango vinne vya lugha ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mtafiti katika utafiti huu atamakinikia viwango viwili tu kati ya hivyo; fonolojia na mofolojia.

### 2.2.1 Fasili ya dhana ya Fonolojia

Massamba (2013:3) anasema kuwa fonolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na kuchunguza mifumo ya lugha mbalimbali za binadamu. Kila lugha ya binadamu ina mfumo wake wa sauti ambao huongoza ujenzi wa maneno ya lugha hiyo. Fonolojia ni taaluma inayotuambia ni sauti zipi zinatumika katika lugha fulani na zipi hazitumiki katika lugha hiyo. Pia taaluma hii hutuelekeza uwezekano wa mfuatano wa sauti katika lugha hiyo, na ni sauti zipi zinaweza kutokea katika mazingira yapi; hutuelekeza ni sauti zipi zinaweza kuungana na kuna mashartizuizi gani. Kwa kuwa lugha zote za binadamu ni asilia na zote hutumia sauti kutoka katika bohari kuu lilelile la sauti bila shaka zitakuwa zinachangia sifa za msingi. Hata hivyo, kwa kuwa kila lugha ina mfumo wake tofauti wa sauti haitawezekana kuwa na lugha mbili

zenye mfumo uleule mmoja wa sauti. Hivyo basi, utafiti huu umechunguza kwa kina jinsi tofauti hizo za kifonolojia zilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu kwa wazungumzaji wa Kisukuma.

### 2.2.2 Fasili ya dhana ya Fonimu

Massamba (2004:12) anasema; fonimu ni kipande kidogo kabisa katika mfumo wa sauti za lugha ambacho kina sifa pambanuzi cha kuweza kukitofautisha na vipande vingine vya aina yake; sauti pambanuzi katika mfumo wa lugha. Naye Mgullu (2012:55) na Riro, (2012:60) wanaeleza kuwa fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha lugha ambacho kina uamilifu wa kutofautisha maana kinapochukua nafasi ya kipashio kingine chenye hadhi sawa. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa fonimu ni kitamkwa katika neno ambalo kikibadilishwa na kitamkawa kingine maana ya neno hilo hubadilika au hupotoka katika lugha hiyo. Kwa maelezo haya ya wataalamu tunapaswa kuelewa mambo mawili ya msingi. Kwanza, fonimu ndio msingi mkuu wa lugha yoyote ile; maana lugha ni sauti hivyo bila ya sauti hakuna lugha. Pili, ingawa maelezo kuhusu dhana ya fonimu yanasisitiza kuwa fonimu hubadilisha maana ya neno; ieleweke kwamba fonimu yenyewe haina maana ila zinapoungana fonimu mbalimbali kwa utaratibu unaokubalika katika lugha husika ndipo maana hupatikana. Hivyo, maana ya neno hubadilika iwapo fonimu moja kati ya fonimu kadhaa zilizowekwa pamoja kuunda neno itabadilika. Katika utafiti huu tathmini na uchunguzi wa namna Kisukuma kinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kifonolojia utahusisha pia fonimu za lugha hizi ambazo ndio zinaunda maneno katika lugha.

### 2.2.3 Fasili ya dhana ya Mofolojia

Besha (2007:49) anasema; mofolojia ni taaluma inayojishughulisha na kuchambua muundo wamaneno katika lugha. Misingi ya wataalamu hawa wawili wanaonekana kuingiliana katika kuonesha namna ya taaluma ya mofolojia inavyojihusisha na muundo wa maneno katika lugha. Mofimu ndiyo kipashio cha msingi katika mofolojia.

Massamba na wenzake (2009:32) wanafasili mofolojia kuwa ni kiwango cha sarufi kinachojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha yaani jinsi maneno ya lugha yoyote ambayo inaundwa.

Massamba (2010) akimnukuu Martinet (1965) ambapo Martinet alinukuu kutoka kwa Trubetzkoy (1929) anaeleza kuwa; mofofonolojia kama ilivyotumiwa na Trubetzkoy ilimaanisha sehemu ya isimu ambayo ingeweza kutumia mofolojia kuelezea tofauti fulani za kifonolojia ambazo zisingeweza kuelezwa kwa kutumia data za kifonolojia peke yake. Mofolojia kama taaluma ya isimu/ sarufi ambayo inalo jukumu la kuyachunguza maneno ili kuyaelewa maneno yake yalivyo.

### 2.2.4 Fasili ya dhana ya mofimu

Massamba na wenzake (2013:13), wanaeleza kuwa Mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika umbo la neno kilicho amilifu (yaani kilicho na kazi ya kisarufi au kileksika) na ambacho hakiwezi kuvunwa au kugawanywa katika vipande vidogo bila kupoteza uamilifu wake.

### 2.2.5 Fonolojia ya Kiswahili

Katika fonolojia ya lugha yoyote iwayo, fonimu ndiyo kipashio cha msingi. Idadi ya fonimu hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine, Kuna mgawanyo bayana wa fonimu za lugha ya Kiswahili, kuna makundi mawili yaliyojikita katika kuangalia namna sauti zitolewavyo ni **Irabu/vokali na Konsonanti.**

#### 2.2.5.1 Fonimu za irabu/vokali za Kiswahili sanifu

Massamba na wenzake (2004) wanasema irabu ni aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa pasi na kuwepo kizuizi chochote katika mkondo wa hewa utokao mapafuni ukipitia katika chemba ya kinywa na chemba ya pua. Hivyo migawanyo ya irabu haitegemei mzuio wa hewa bali hutegemea sana mkao wa ulimi katika kinywa wakati wa utamkaji, na pia mkao wa midomo wakati huo. Kwa sababu hizi, irabu hupangwa kufuatana na vigezo vitatu: ulimi uko juu kiasi gani kinywani (ujuu), ni sehemu gani ya ulimi inainuliwa au kushushwa (umbele) na midomoikoje wakati huo (uviringo).

**Ujuu**

Wakati wa kutamka irabu-juu ulimi unakuwa umeinuliwa juu katika kinywa, ambapo irabu- chini hutolewa wakati ulimi umeteremshwa chini. Irabu-juu ni kama [i,u] na irabu-chini ni kama [a]. Ulimi ukiwa katikati ya kinywa, irabu zinazotolewa huitwa irabu-kati, nazo ni kama [e, o].

**Umbele**


Wakati ulimi unainuliwa kinywani, unaweza kupelekwa mbele katika kinywa na hivyo kutolewa irabu-mbele kama [i, e]. Ikiwa ulimi utarudishwa nyuma, basi irabu

zitolewazo zitakuwa irabu-nyuma kama [u, o]. Irabu [a] kama ya Kiswahili hutolewa ambapo ulimi hauko mbele au nyuma, bali uko katikati.

**Uviringo**

Wakati wa utamkaji wa irabu midomo inaweza kuviringwa, na irabu zitakazotolewa zitakuwaviringo kama [u, o]. Midomo inaweza kusambazwa au kupanuliwa na hivyo kutoa irabu siviringo, kama [i, e, a].

**KIELELEZO CHA IRABU ZA KISWAHILI**




/i/ irabu juu mbele siviringo

/u/ irabu juu nyuma viringo

/e/ irabu kati mbele siviringo

/o/ irabu kati nyuma viringo

/a/ irabu chini siviringo

Chanzo: Massamba na wenzake (2004)

**2.2.5.2 Viyeyusho/fonimu za nusu irabu za Kiswahili sanifu**

Ni aina ya vitamkwa/fonimu ambavyo si konsonanti na wala si irabu; yaani ni vitamkwa ambavyo huchukuliwa kuwa viko katikati ya irabu na konsonanti. Kwa

vile vitamkwa hivi havina sifa kamili ya ukonsonanti na pia havina sifa kamili uirabu lakini vinaelekea zaidi kufanana na irabu wakati mwingine hupewa jina la nusu-irabu. Katika lugha nyingi zakibantu viyeyusho huwa ni vya aina mbili: [j] na [w].

### 2.2.5.3 Fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu

Massamba na wenzake (2004:27) wanasema konsonanti ni aina za sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo wa hewa utokao mapafuni kupitia chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje, uzuiaji wa mkondo huo wa hewa unaweza kuwa wa kubana kabisa na kuachiwa ghafla au kuachia taratibu mfano [p], pia unaweza kuwa wa kubana kabisa na kisha kuachiwataratibu mfano [ch], [t].

Kuna aina mbili kuu za sauti za konsonanti: sauti ghuna (konsonanti zinapotamkwa, hewa **hutikisa** nyuzi za sauti) na sauti sighuna (konsonanti zinapotamkwa, hewa **haitikisa** nyuzi za sauti), kama inavyoonekanika hapo chini katika jedwali la vitamkwa vya konsonati vya Kiswahili.

**Jedwali Na. 2.1 Vitamkwa konsonanti vya kiswahili**

| JINSI/NAMNA YA MATAMSHI | MAHALI PA MATAMSHI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MIDOMO | MIDOMO MENO | MENO | UFIZI | KAAKAA GUMU | KAAKAA LAINI | KOROMEO |
| VIPASUO | GHUNA | b | | | d | | g | |
| | SIGHUNA | p | | | t | | k | |
| | MPUMUO | $p^h$ | | | $t^h$ | $y^h$ | $k^h$ | |
| VIZUIO KWAMIZI | GHUNA | | | | | f | | |
| | SIGHUNA | | | | | č | | |
| VIKWAMIZI | GHUNA | | v | ð | z | | ɣ | h |
| | SIGHUNA | | f | Ɵ | s | š | | |
| NAZALI/ | GHUNA | | | | n | ɲ | d | |
| VING'ONG'O | SIGHUNA | | | | | | | |
| VITAMBAZA | GHUNA | | | | | | | |
| | SIGHUNA | | | | I | | | |
| VIMANDENDE | GHUNA | | | | r | | | |
| | SIGHUNA | | | | | | | |
| VIYEYUSHO | GHUNA | | | | | | | |
| | SIGHUNA | w | | | | y | (w) | |

**Chanzo:** Massamba na wenzake (2004: 44)

Kwa mujibu wa Massamba na wenvzake, jedwali hili linaonesha kuwa Kiswahili kina jumlaya fonimu konsonanti 30. Miongoni mwa fonimu hizo 30 ghuna ni 21 na 9 si ghuna.

#### 2.2.5.4 Miundo ya silabi katika lugha ya Kiswahili

Feng Shengli, (2003) anafasili silabi kuwa ni mpangilio wa fungu la sauti za kutamkwa. Akifafanua zaidi dhana ya silabi Crystal, (2003) anasema silabi kuwa ni sauti moja au zaidi inayowakilisha kifungu kimoja cha sauti katika lugha. Massamba na wenzake, (2004) Silabi ni sehemu ya neno ambayo huweza kutamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Maelezo haya yanamaana kwamba maneno ya lugha hutamkwa katika utaratibu wa kufuata silabi. TUKI (2004-2005) wanaeleza kuwa, silabi ni sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake na kutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Kwa mfano, “i” na “ta” katika neno “ita” ni silabi mbili tofauti. Hivyo basi kwa kuangalia maana zilizotolewa na wataalamu mbalimbali tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho sauti au fungu la sauti linalojitosheleza kimatamshi, hutamkwa mara moja na kwa pamoja.

Kwa mujibu wa Kihore (2003), katika lugha ya Kiswahili kuna miundo mbalimbali ya silabi, kwanza kabisa kuna miundo ya silabi zinazotokana na lugha za kibantu ambayo ni kama ifuatavyo;

**Muundo wa irabu peke yake (I).**

Mifano;

Ua-/u//a/

Oa-/o//a/

**Muundo wa silabi konsonanti na irabu (KI).**

Mifano;

Kama-/ka//ma/

Baba-/ba//ba/

**Muundo wa silabi ya konsonanti, kiyeyusho na irabu (KKI).**

Mifano;

Fyeka-/fye/ka

Bweka-/bwe/ka

**Muundo wa silabi ya nazali peke yake.**

Mifano;

Nne-/n/ne

Nchi-/n/chi

**Muundo wa silabi wa konsonanti, konsonanti na irabu (KKI),** katika muundo huu wasilabi konsonanti ya mwanzo huwa ni vitamkwa nazali [m] na [n].

Mifano;

Ngamia-/nga/mi a

Ndama-/nda/ma

**Muundo wa silabi wa konsonanti, konsonanti, kiyeyusho na irabu (KKKI).**

Mifano;

Jangwa-ja/ngwa/

Ugonjwa-u go/njwa/

Kwa mujibu wa Samwel (2009), Miundo ya silabi za Kiswahili zinazotokana na maneno yalugha za kigeni ni pamoja na;

**Muundo wa konsonanti, konsonanti na irabu (KKI),** muundo huu ni tofauti na muundouliotangulia kwani muundo huu unahusisha tu konsonanti zisizokuwa nazali.

Mifano;

Labda (Kiajemi)-la/bda/

Stoo (Kiingereza)-/sto/o

**Muundo wa silabi wa konsonanti, konsonanti, konsonanti na irabu (KKKI),** muundo huu nao unajitokeza katika lugha ya Kiswahili sanifu kutokana na maneno ya mkopo kutoka lugha ya kiingereza.

Mifano;

Springi-/spri/ngi

Skrubu-/skru/bu

**Muundo wa silabi wa konsonanti, irabu na konsonanti**. Kuna maneno yenye asili ya kigeni katika lugha ya Kiswahili sanifu ambayo yana silabi funge na yana muundo wa konsonanti, irabu na konsonanti. (KIK).

Mifano;

Maktaba-/mak/ta ba

Muktadha-/muk/ta dha

**Muundo wa silabi ya irabu na konsonanti (IK).**

Mifano;

Oksijeni-/ok/ si je ni

Inspekta-/in/spek ta

**Muundo wa silabi wa konsonanti, konsonanti, irabu na konsonanti (KKIK).**

Mifano;

Trekta-/trek/ ta

Inspekta-in /spek/ ta


Kwa muhutasari, maandiko tuliyoyapitia kuhusu fonolojia ya Kiswahili yametusaidia kufahamu namna maneno ya lugha sanifu ya Kiswahili yanavyotamkwa na mahali pakutamkia, pia miundo mbalimbali ya silabi za Kiswahili sanifu yameainishwa.

### 2.2.6 Fonolojia ya kisukuma

Kama ilivyo kwenye Kiswahili, fonolojia ya Kisukuma nayo inajumuisha sauti za aina mbili; konsonanti na irabu. Ufafanuzi wa sauti hizo katika Kisukuma ni kama ifuatavyo:

#### 2.2.6.1 Dhana ya Irabu katika lugha ya Kisukuma

Migawanyo ya irabu haitegemei mzuio wa hewa bali hutegemea sana rnkao wa ulimi katika kinywa wakati wa utamkaji, na pia mkao wa midomo wakati huo. Kwa sababu hizi, irabu hupangwa kufuatana na vigezo vitatu: Ulimi uko juu kiasi gani kinywani (ujuu); ni sehemu gani ya ulimi inainuliwa au kushushwa (umbele); na midomo ikoje wakati huo (uviringo).




/a/ +irabu

+ kati

+chini

-mviringomfano:

abhana- watoto Abhizikulu - wajukuu

/e/ + irabu

+mbele

+nusu chini

–mviringo

mfano:

Bhebhe – wewechene –chini

/I/ +irabu

+mbele

–mviringo

+nusu juu

mfano:

Ijagi –jagiIdatu- tatu

/i/ + irabu

+mbele

-mviringo

+ juu

mfano: ipela – peraidoka – duka

idoke -mgomba

/ ʊ/+ irabu

+nyuma

+mviringo

+nusu juu

mfano: idatʊ– tatuʊleja - unaenda ʊlelya – unakula?

/u/ + irabu

+juu

+nyuma

+mviringo

Mfano: mabhu-majivu

Irabu za lugha ya Kiswahili na lugha ya Kisukuma kwa kiwango kikubwa zinafanana sana, irabu ya lugha Kisukuma na irabu za lugha ya Kiswahili zote zinaonesha kwa baadhi ya irabuzao zina mviringo na pia kutokuwa na mviringo

| Irabu ya lugha ya Kiswahili | Irabu ya lugh aya Kisukuma |
|---|---|
| /i/ juu mbele, si mviringo | /i/ mbele, nusu juu, si mviringo |
| /u/juu, nyuma, mviringo | /u/juu, nyuma, mviringo |
| /e/kati nyuma, si mviringo | /e/mbele, nusu chini, si mviringo |
| /o/kati nyuma, mviringo | /o/nyuma, nusu juu, mviringo |
| /a/ chini, si mviringo | /a/kati, chini, si mviringo |

Chanzo: ruhuwiko.blogspot.com

**2.2.6.2 Dhana ya konsonanti katika lugha ya Kisukuma**

Massamba na wenzake (2004: 27) Konsonanti ni aina za sauti ambazo hutambulika kama kuzuia mkondo wa hewa utokao mapafuni kupitia chemba cha kinywa na chemba ya pua kuondoa nje uzuiaji wa mkondo huo wa hewa unaweza kubana kabisa au kuachiaghafla kisha kuachia taratibu kama tunatamka neno /p/.

Naye Masebo (2012:89) anaeleza Konsonanti ni sauti zinazotamkwa kwa kuzuia mkondo wa hewa katika sehemu mbalimbali hasa kwa kutumia ulimi kama vile /p/, /b/ /d/.

Kutokana na fasili hizo tunaona kwamba kuzuiwa mkondo hewa ni jambo la msingi sana katika kuzitambulisha sauti za konsonanti. Kila konsonanti hutambuliwa kwa kuangalia ni ala gani zimetumika kuzuwia mkondo hewa na namna hewa hiyo inavyoruhusiwa kutoka nje.

Katika lugha ya kisukuma tunapata Konsonanti zifuatazo kama zinavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:

**Jedwali Na. 2.2 Konsonanti zipatikanazo katika lugha ya kisukuma**

| JINSI/NAMNA YA MATAMSHI | MAHALI PA MATAMSHI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MIDOMO | MIDOMO MENO | MENO | UFIZI | KAAKAA GUMU | KAAKAA LAINI | KOROMEO |
| VIPASUO | GHUNA | bh | | | d | | g | |
| | SIGHUNA | p | | | t | | k | |
| | | | | | | | | |
| VIZUIO KWAMIZI | GHUNA | | | | | f | | |
| | SIGHUNA | | | | | Č | | |
| VIKWAMIZI | GHUNA | | v | ð | z | | ɣ | h |
| | SIGHUNA | | f | Θ | s | Š | | |
| NAZALI/ VING’ONG’O | GHUNA | m | | | n | ɲ | a | |
| | SIGHUNA | | | | | | | |
| VITAMBAZA | GHUNA | | | | | | | |
| | SIGHUNA | | | | I | | | |
| VIMANDENDE | GHUNA | | | | r | | | |
| | SIGHUNA | | | | | | | |
| VIYEYUSHO | | w | | | | y | (w) | |

**Chanzo:** learningtz.blogspot.com

Kwa kiwango kikubwa katika lugha ya Kiswahili konsonanti hujitokeza katka aina mbili za sauti yaani, sauti ghuna (konsonanti zinapotamkwa, hewa hutikisa nyuzi za sauti) na sauti sighuna (konsonanti zinapotamkwa, hewa haitikisa nyuzi za sauti), lakini katika lugha ya Kisukuma aina ya sauti ambayo hujidhihirisha zaidi ni sauti ghuna kwa sababu utamkaji katika lugha hiyo hutumia mkazo sana katika kutamka maneno.

### 2.2.6.3 Miundo ya silabi katika lugha ya Kisukuma

Riro (2012: 77) anafasili silabi kuwa ni dhana ya kifonolojia ambayo huwakilisha umbo la matamshi ambapo sauti moja au zaidi hutamkwa kwa mara moja kama fungu moja la sauti. Ifuatayo ni Miundo ya silabi katika lugha ya kisukuma

i) Muundo wa Irabu peke yake (I)

mfano: Ipela – pera

Idatu – tatu

Enzoka – nyoka

Aho – pale

ii) Muundo wa Konsonanti + Irabu (KI)

mfano:

Sekaga - cheka

Tolaga – oa

Somaga – soma

iii) Muundo wa konsonanti + konsonati +Irabu (KKI)

mfano:

Embiti – fisi

Ngosha- mwanaume

Chagulaga – chagua

Ntale - mkubwa

Ndoke – ndizi

iv) Muundo wa konsonanti+ kiyeyusho+ Irabu (KI1/2 I)

mfano:

Ulelya - kula

Nyanza – ziwa

v) Muundo wa konsonanti peke yake (K)

mfano:

Mva- mbwa

vi) Muundo wa Konsonanti + Konsonanti + kiyeyusho + Irabu (KKI1/2 I)

Mfano;

Nsungwi- sungwi

Ngwala – Ngwara

Kwa ujumla miundo ya silabi za lugha ya Kiswahili na Kisukuma inafanana katika namna miundo hiyo inavyo undwa kama vile muundo wa irabu peke yake, muundo wa irabu na konsonanti, muundo wa konsonanti peke yake. Hata hivyo kazi tangulizi hizo zote zimemwezesha mtafiti kuweza kubaini athari za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kisukuma kwa mwanafunzi anayejifunza Kiswahili sanifu.

### 2.2.6.4 Athari ya lugha za Kibantu katika lugha ya Kiswahili

Tafiti mbalimbali zimekuwa zikifanyika juu ya athari za lugha za Kibantu katika lugha ya Kiswahili. Ingawa kumekuwa na jitihada za kuimarisha lugha ya Kiswahili, tafiti nyingi zinaonesha kuwa wazungumzaji wengi wa lugha za kikabila wamekuwa wakifanya makosa mengi wakati wanapotumia lugha ya Kiswahili pindi wanapofanya mazungumzo yao. Baadhi ya makosa hayo yamekuwa katika viwango tofauti tofauti kama vile makosa ya kimofolojia, kifonolojia, kisintaksia na kisemantiki.

Nyanda (2015) alichunguza athari za lugha ya Kinyamwezi Katika kujifunza lugha ya Kiswahili ambapo matokeo ya uchunguzi huo yamedhihirisha athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Athari hizo ni pamoja na ndimi za wazungumzaji wa Kinyawezi kuathiriwa na lugha mama kwa kukosekana kwa sauti / r /,/ γ /,/ ϴ / na / ð / na / b / katika lugha ya Kinyamwezi, kukosekana kwa baadhi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kinyamwezi, ufundishaji mbaya wa walimu wa lugha ya Kiswahili. Vilevile wanafunzi kutopata muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili wawapo nje ya mazingira ya shule na Wazazi na watoto wao kutoona umuhimu wa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili.

Wenceslaus (2015) naye alichunguza athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa athari za matamshi zinazojitokeza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili ni pamoja na udondoshaji wa sauti, kutumia sauti zinazokaribiana na kuongeza viambishi visivyohitajika. Aidha Wenceslaus (khj) anafafanua kuwa watoto wanatakiwa

wafundishwe Kiswahili tangu wadogo na wazazi wawe mfano wa kuzungumza Kiswahili.

Vilevile, Msangi (2016) anaelezea athari za lugha za Kimakabila kwenye elimu yetu[1] anadai kuwa japokuwa lugha za makabila zinatambulisha tamaduni zetu na kuonesha asili zetu na hata kuwa marejeo katika tafiti kwa baadhi ya masomo lakini haitambuliki kama lugha ya kujifunzia au kufundishia. Hivyo basi, tafiti mbalimbali zimebainisha athari ya lugha za makabila katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu, hata hivyo ipo haja pia ya kuchunguza namna Kisukuma kinavyoathiri Kiswahili sanifu na kutathmini athari zipi zinatawala zaidi ya nyingi kwa athari za kifonolojia na kimofolojia. Kwa hiyo, utafiti huu umeziba pengo hilo la maarifa kwa kuchunguza na kutathmini athari za lugha ya Kisukuma kimofolojia na kifonolojia katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

### 2.2.7 Kiunzi cha nadharia

Ili utafiti ufanyike kwa uaminifu na uthabiti wenye kutoa faida inayotarajiwa kulingana na lengo la utafiti huo, ni lazima utafiti huo uongozwe na nadharia sahihi kwani nadharia hiyo hubeba dhana, mawazo au malengo yatolewayo kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, muundo, chanzo au utendaji wa jambo. Dhana ya nadharia imejadiliwa na wanazuoni mbalimbali ambao wamekuja na mitazamo tofauti tofauti kama ifuatavyo;

Wamitila (2003:22) anasema nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kueleza hali fulani, chanzo chake, muundo wake, utenda kazi wake na mwingiliano

[1] www.tujue.blogspot.com/2016/12/lugha-za-kimakabila-zina-athari-kwenye.htl?m

wake wa ndani na nje. TUKI (2004:300) wanasema nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza jambo fulani. Fasili hii ya TUKI inafanana kwa kiasi fulani na ile ya Mdee (2011) anayefasili nadharia kuwa ni mpango wa maneno uliotungwa ilikueleza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Kwa msingi huo nadharia hubeba mawazo, dhana au maelezo yatolewayo kwa nia au lengo la kueleza hali fulani, chanzo, muundo, utendaji na mwingiliano wa ndani na nje.

Mtafiti ameteua nadharia ya Uchanganuzi Linganishi kwa sababu ina uwezo wa kushughulikia ulinganifu wa lugha mbili kama ilivyoangaziwa. Nadharia hii iliasisiwa mwanzoni na Fries (1945) kisha baadaye ikapambanuliwa na Lado (1957). Spolsky (1989), anasema nadharia ya Uchanganuzi Linganishi iliibuliwa na kuongezewa vipengele vya Sarufi Jumulifu. Inapotumika huonesha zaidi uwiano na tofauti kati ya lugha mbili. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ina mihimili ifuatayo: Kwa mujibu wa Lado (1957), katika ujifunzaji wa lugha kuna ugumu na vizuizi. Kiini au sababu kuu ya ugumu na kutokea kwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili inatokana na uhamishaji wa dhana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Kulingana na Weinreich (1953), upo uwezekano wa kukisia na kutabiri ugumu na makosa wakati wa kujifunza lugha ya pili kutokana na tofauti zinazopatikana kati ya lugha mbili husika lli kurahisisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili, tofauti kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili hubainishwa ili ishughulikiwe ipasavyo wakati wa kujifunza kwa kutiliwa mkazo. Imebainika kuwa mihimili hiyo inaweza kutumika katika utafiti huu. Mtafiti ameteua nadharia hii kwa sababu kuna hali ya kulinganisha na kulinganua athari za lugha ya Kisukuma

zinazohusu lugha ya Kiswahili sanifu katika vipengele vya kisarufi kama kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Mihimili ambayo itaongoza utafiti huu ni kama ilivyoelezwa hapa chini:

Kutoa taratibu za lugha mbili zitakazolinganishwa ili uwiano na tofauti ibainishwe. Kutenga tofauti zikishabainishwa, kwani itakuwa rahisi kutambua vipengele ambavyo huenda vikasababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili , Spolsky (1989), anasema mwalimu na mwanafunzi wakibaini uwiano na tofauti kati ya taratibu mbili za lugha husika itakuwa rahisi kugundua na kubainisha vipengele ambavyo vinastahili kutiliwa mkazo ili kurahisisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili Nadharia hii imechukuliwa kuwa makisio yanaweza kutolewa pamoja na maelezo juu ya muundo ambao unaweza kusababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ellis (1985), anatoa utaratibu wa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi na ni kama ufuatavyo:

Kutoa maelezo juu ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ambapo kwa muktadha wa kazi hii ni lugha ya Kisukuma na Kiswahili. Kufafanua vipengele vya kisarufi vitakavyoteuliwa na kushirikishwa katika uchunguzi yaani kimofolojia, kifonolojia na kisemantiki.

Kudhihirisha mpangilio wa matamshi, maumbo, na maana. Kulinganisha na kulinganua uwiano na tofauti kati ya lugha mbili husika. Kukisia na kutabiri vipengele vinavyoweza kusababisha matumizi ya sarufi mbaya. Kama ambavyo tumeelezea hapo juu, maelezo ya tafsiri yametolewa kuhusu taratibu hizo za ujifunzaji. Maelezo yameshirikisha vipengele vya kisarufi: kifonolojia, kimofolojia,

kisemantiki pamoja na mbinu za kufunzia lugha. Palipo na tofauti ndipo pamechukuliwa kuwa kiini kinachosababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hivyo basi walimu wamehimizwa kuzingatia palipo na tofauti wanapofunza. Kutokana na maelezo ya utaratibu wa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imebainika kuwa hii nadharia ni mwafaka kwa utafiti huu. Nadharia hii imeundwa kwa lengo la kuchunguza ugumu ambao wanafunzi walio na lugha yao ya kwanza hupata wanapojifunza lugha ya pili. Haya yameafikiana na madhumuni ya utafiti huu kwani kuna lugha mbili zinazolinganishwa (Kisukuma na Kiswahili).

Hata hivyo nadharia hii ya Uchanganuzi Linganishi imelaumiwa kwa kuwa na mtazamo finyu kuhusu ujifunzaji wa lugha. Kwa mujibu wa Weinrech (1953), kuna madai kuwa nadharia hii huangazia njia moja tu ya kujifunza lugha ambayo ni uhamishaji wa dhana hasi. Msemaji anapoitumia lugha ya pili, hujikuta ameyatumia maneno anayoyaelewa na kuyazoea katika lugha yake ya kwanza. Nadharia hii hutilia maanani hatua na mapito apitiayo mwanafunzi anapoanza kujifunza lugha hadi anapoijua kiasi cha kuupata umilisi. Ellis (1985) anashikilia kuwa suala la kutabiri makosa yasiyokuwepo limepingwa kwani utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa wanafunzi hujaribu kukwepa kuturnia maneno magumu wanapojifunza. Anasema kuwa makosa ya wanafunzi kati ya theluthi moja na nusu hutokana na athari ya lugha zao za kwanza. Hata hivyo imebainika kuwa lengo kuu la Uchanganuzi Linganishi ni kuangalia nafasi ya lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili wala sio kutabiri makosa yasiyohusishwa na mwanafunzi. Isitoshe hata nadharia hiyo ya kuchanganua makosa pia inayo upungufu kama vile kutotoa picha kamili ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Inayo mazoea ya kujikita tu kwa makosa badala

ya kuzingatia uwezo alio nao mwanafunzi katika utendakazi. Vile vile, upungufu mwingine ni kuwa nadharia hiyo haina uwezo wa kutabiri makosa ambayo anaweza kuyafanya mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili.

## 2.3 Muhtasari

Sura hii imejadili kwa ujumla dhana muhimu za kisarufi ambazo zitatumika katika utafiti huu. Mtafiti amebainisha vipengele vya kifonolojia na kimolfolojia vitakavyochunguzwa na kujadiliwa. Vilevile sura hii imebainisha tafit tangulizi kuhusu athari ya lugha za Kibantu katika Kiswahili sanifu. Kiunzi cha nadharia ambacho kimetumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data pia kimefafanuliwa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti na usampulishaji, ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Katika utafiti, ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data hufaywa kwa kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala wa kitaamuli. Kwa mujibu wa Williman (2011), mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kukusanya na kuchambua data ambayo mtafiti hutumia namba kurekodi taarifa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu, kwa mfano achano sanifu. Aidha Kress (2008), anafafanua mkabala wa kitaamuli kuwa, unaelezea vipi na kwa nini matukio yametokea. Hivyo utafiti huu umetumia mkabala wa kitaamuli katika ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data. Mkabala wa kitaamuli umetumika ili kuweza kupata maeezo ya kina juu ya tathmini na uchunguzi wa athari ya lugha ya Kiswahili katika ujifunzajia wa lugha ya Kiswahili sanifu. Data zilizopatikana ziliwasilshwa kwa kutumia maelezo na jedwali kwa njia ya asilimia.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Kabla ya kuanza kufanya ukusanyaji wa data ni vyema kuchagua mahali ambapo upatikanaji wa data utatosheleza majibu ya maswali ya utafiti ili kufanikisha lengo la utafiti. Uchunguzi ulijikita katika mkoa wa Tabora, wilaya ya Tabora mjini hususani katika shule za msingi Mwenge, Isike, Mihayo na Kitete. kwa sababu ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kufika sehemu lengwa kwa urahisi kutokana na miundo mbinu

rahisi ya usafiri, watafitiwa lengwa (wanafunzi wanaojua lugha ya kisukuma, wazee wanaojua lugha ya kisukuma na Kiswahili walipatikana eneo hilo kwa urahisi.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa ni wazungumzaji na wataalamu wa lugha ya Kiswahili na Kisukuma. Kothari (2004) anasema kuwa uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti atatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Walengwa watakaohusishwa katika utafiti huu ni wanafunzi kutoka shule nne za msingi zilizopo katika Mkoa wa Tabora hususani Wilaya ya Tabora mjini ambazo ni Shule ya msingi Mwenge, Shule ya msingi Isike pamoja na walimu wa Kiswahili wanaofundisha katika shule hizo.

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kulingana na sifa na umuhimu wa kila kundi katika utafiti huu. Sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo husaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Watoa taarifa ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya utafiti kurejelea watu au vitu vinavyoteuliwa na kuchaguliwa na mtafiti kwa ajili ya kufanyia utafiti wake kwa kuzingatia aina na malengo ya utafiti anaokusudia kufanya (Kothari 2004). Kwa mfano, wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili katika shule zilizoteuliwa wanajua lugha ya Kisukuma ambayo ni lugha yao ya kwanza na wanajifunza Kiswahili shuleni ambapo Kiswahili kinafundishwa kama somo. Hivyo basi utafiti huu uliliona kundi hili kuwa ndilo lenye uwezo wa kutoa data juu ya athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza Kiswahili. Walimu waliteuliwa kwa sababu wanafundisha somo hilo hivyo ni rahisi kutoa data halisi kulingana na mahojianao kutoka kwa mtafiti na wazee kwa

sababu wao wana umilisi wa lugha ya asili ya Kisukuma na Kiswahili hivyo ni rahisi kutoa data halisi kulingana na mahojianao na hoaji kutoka kwa mtafiti.

Hata hivyo, kwa kuwa si rahisi kukusanya taarifa kutoka kwenye kundi lote la wanafunzi na walimu, usampulishaji kusudio na usampulishaji nasibu umetumika katika kuteua sampuli ya watoa taarifa wa utafiti huu. Usampulishaji kusudio umetumika katika kuteua shule na walimu na usampulishaji nasibu umetumika kuteua wanafunzi walio wawakilisha wanafunzi wenzao. Mtafiti ametumia wanafunzi 36 kwa wanafunzi watatu kutoka katika kila darasa kwa shule zote zilizoteuliwa. Pia ameteua walimu wa Kiswahili wanne, mwalimu mmoja kutoka katika kila shule na wazee wanne kutoka maeneo ya Tabora mjini, kama inavyoonekana katika Jedwali 3.1. Makundi hayo yaliyoteuliwa yamemsaidia mtafiti kujibu maswali yaliyolengwa katika malengo ya utafiti huu.

**Jedwali Na. 3.1 Mgawanyo wa Sampuli**

| **Walengwa** | **shule** | **idadi** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Wanafunzi darasa la 5 | Isike<br>Mwenge<br>Mihayo<br>Kitete | 3<br>3<br>3<br>3 | 12 |
| Wanafunzi darasa la 6 | Isike<br>Mwenge<br>Mihayo<br>Kitete | 3<br>3<br>3<br>3 | 12 |
| Wanafunzi darasa la 7 | Isike<br>Mwenge<br>Mihayo<br>Kitete | 3<br>3<br>3<br>3 | 12 |
| Walimu | Isike<br>Mwenge<br>Mihayo<br>Kitete | 1<br>1<br>1<br>1 | 4 |
| Wazee | Tabora mjini (mtaa wa chuo cha nyuki) | 4 | 4 |
| | | JUMLA | 44 |

Katika jedwali hilo mtafiti aliteuwa wanafunzi wa darasa la tano, sita na saba kwa sababu walikuwa na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha, na pia waalimu wa Kiswahili waliteuliwa kwa sababu walikuwa na ujuzi wa lugha hiyo ya Kiswahili, na wazee kwa sababu wanaumilisi wa lugha ya kisukuma na Kiswahili.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Katika masuala yautafiti kuna data za aina mbili, data za msingi na data fuatizi au data za upili. Data za msingi ni data halisi ambazo zinakusanywa na mtafiti kwa mara ya kwanza. Kufanya utafiti maskanini kulimwezesha mtafiti kukusanya data mbalimbali zitakazohusu mada ya utafiti katika maskani mbalimbali. Berg (2007) anasema maskani ni mahali ambapo watu wanaishi na mtafiti anapokwenda kutafuta kupata data ambazo ni mpya, halisi ghafi ambazo hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa ajili ya utafiti kama wake. Hivyo katika utafiti huu mtafiti amekusanya data za msingi kutoka kwa watoa taarifa walioteuliwa.

#### 3.5.1 Mbinu za kukusanyia Data

Kombo na Tromp (2006) wameeleza kuwa, ukusanyaji wa data unahusu kukusanya taarifa mahususi zilizokusudiwa kutoa au kupinga uhalisia wa mambo fulani. Mtafiti anatakiwa kuteuwa kwa makini mbinu za ukusanyaji wa data ambazo zikitumiwa vizuri zitawezesha kufanikiwa kwa lengo lililokusudiwa na mtafiti. Msaghaa (2010) anasisitiza kuhakikisha kuwa mbinu au njia za kukusanyia data zinatoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu swali la utafiti. Utafiti huu umetumia mbinu ya hojaji na mahojiano kwa watoa taarifa walioteuliwa.

### 3.5.1.1 Mahojiano

Kothari (2008) anasema hii ni njia ya kupata data kwa kutumia maswali na majibu yanayofanywa kwa mazungumzo kati ya mtafiti na mtoa taarifa. Mbinu hii ilitumika kwakwa wanafunzi wa shule za msingi. Mahojiano hayo yalifanyika punde tu baada ya watoa taarifa kumaliza kujaza hojaji. Mbinu hii iliteuliwa kwa sababu ya kupata uthabiti wa majibu ya watoa taarifa pamoja na kupata uthabiti wa mbinu za kukusanyia data. Pili, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli kwa usahihi zaidi. Hii iliwezekana kwa sababu mtafiti alikutana na wahojiwa ana kwa ana, na kuwauliza maswali; maswali yaliyo kosa majibu yalitafutiwa ufumbuzi papo kwa papo. Tatu ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi, kwa sababu watoa taarifa waliweza kuuliza maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali zaidi ambayo ni vigumu kufanyika kwa kutumia mbinu nyingine kama vile ushuhudiaji, ushiriki au hojaji. Mbinu hii ilisaidia katika uchanganuzi wa data za kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza Kiswahili sanifu.

### 3.5.1.2 Mbinu ya hojaji

Mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti huandaa maswali kuhusiana na jambo fulani. Williman (2011) anaeleza kuwa, kuna maswali ya hojaji ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa wa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia, inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ni maswali ya hojaji yasiyofunge, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua. Aidha, husaidia kupata taarifa nyingi zaidi. Mbinu ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu

ilijumuisha aina zote mbili za maswali yaliyokuwemo katika hojaji, maswali funge na maswali yasiyofunge. Mtafiti alichanganya aina zote za maswali ili kuepuka mapungufu yaliyoweza kutokea katika mbinu hizi mbili, ikizingatia kuwa kila moja ina mapungufu yake. Hivyo, mbinu hizo zikitumika kwa pamoja kila moja husaidia kuziba mapungufu ya nyenzie. Mtafiti aliwapa watoa taarifa wanafunzi hojaji wajaze papo kwa papo na walimu walipewa muda wa siku mbili kisha wakarejesha kwa ajili ya uchambuzi wa data. Walimu walipewa muda mrefu kujaza hojaji kwa kuwa walikuwa na majukumu mengi ya kazi, hivyo haikuwezekana kuzipata data iwapo wangetakiwa wajaze papo kwa papo. Mbinu ya hojaji ilichaguliwa kwa sababu ilifaa kukusanya data katika kundi kubwa la watu na kwa muda mfupi sana hasa hojaji za papo kwa papo. Data iliyotarajiwa kupatikana ni pamoja na athari za kimsamiati na kimatamshi iliyosababishwa na Kisukuma katika kujifunza Kiswahili na data iliyopatikana ilisaidia kukamilisha majibu ya athari zipi za kimofolojia na kifonolojia ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Pia mtafiti aliweza kutathmini ni athari zipi zinajitokeza zaidi kuliko nyingine.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechanganuliwa kwa njia ya maelezo. Kwa kuzingatia malengo ya utafiti data zilizokusanywa kutoka kwa watoa taarifa zimegawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanaza likihusisha athari za kifonolojia ya lugha ya Kisukuma katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu na kundi la pili likihusisha data za athari za kimofoljia za Kisukuma katika kujifunza Kiswahili. Vilevile data za makundi hayo mawili zimetumiwa katika kutathmini ni athari zipi zinajitokeza zaidi. Uchanganuzi huo wa data umefanywa kwa kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi

linganishi kwa kulinganisha vipengele vya kifonolojia na kimofolojia katika Kisukuma na Kiswahili kwa wazungumzaji wa Kisukuma wanaojifunza Kiswahili.

### 3.7 Maadili ya Utafiti

Maadili ni kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na jamii ili zitumike kuongoza mwenendo wa maisha na tabia halisi ya maisha ya mwanajamii husika (Mligo, 2012). Maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri, yaani mtafiti hatatoa siri ya mtafitiwa, Mtaalamu huyu pia ameeleza kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu na pia haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Katika utafiti huu mtafiti amezingatia maadili ya utafiti wakati wa ukusanyaji data. Mtafiti alikuwa na kibali cha kukusanya data ambacho ailikwasilisha katika mamlaka za Mkoa wa Tabora na Wilaya. Kwa watoa taarifa, kabla ya kuwapatia hojaji na kufanya mahojiano, mtafiti aliwaeleza watoa taarifa malengo ya utafiti wake na kuwahakikishia kuwa yale yote watakayoeleza yatatumiwa kwa utafiti huu tu na si vinginevyo. Aidha, mtafiti aliwaruhusu watafiti ambao hawakuwa tayari kutoa taarifa wanawea kujitoa katika kundi la watoa taarifa.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amebainisha mkabala wa utafiti, eneo la utafiti na sampuli ya watoa taarifa na namna watoa taarifa hao walivyopatikana. Pia sura imefafanua aina ya data iliyokusanywa na njia zilizotumika kukusanya data ya utafiti huu. Mtafiti pia amebainsha namna alivyozingatia maadili ya utafiti katika ukusanyaji wa data kutoka kwa watoa taarifa.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura inahusu uwasilishaji wa data; na uchambuzi wa data. Data zilizowasilishwa na kuchambuliwa katika sura hii zinatokana na taarifa zilizopatikana kupitia mahojiano nahojaji wakati wa ukusanyaji wa data kutoka katika makundi mawili. Makundi hayo ni walimu na wanafunzi ambao ni wamilisi wa lugha ya Kisukuma. Utafiti ulifanikiwa kukusanya data zilizohusiana na mada ya utafiti kwa kupitia jumla ya watoa taarifa 44. Katika idadi hii, Walimu walikuwa 8 wanafunzi wanaozungumza Kisukuma na wanajifunza lugha ya Kiswahili walikuwa 36. Data zimewasilishwa na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na malengo mahususi ya utafiti ambayo ni kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu, kuchunguza athari za kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu na kutathmini kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Aidha uchanganuzi wa data umefanywa kwa kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganishi.

## 4.2 Athari za Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili Sanifu

Lugha mama ina athari nyingi wakati wa kujifunza lugha nyingine. Mtu anayejifunza lugha ambayo ni mpya kwake, hukumbana na vikwazo na changamoto nyingi zinazoweza kumtatiza na kumzuia wakati wa kujifunza lugha hiyo. Katika utafiti huu mtafiti alibaini athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu. Athari hizi ni za kifonolojia, kimofolojia.

### 4.2.1 Athari za Kifonolojia

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu. Athari za kifonolojia ni athari zote ambazo zinaathiri matamshi au sauti (fonimu) za lugha mahususi. Katika utafiti huu watoa taarifa wameeleza kuwa, athari kubwa ya kifonolojia inaletwa na lugha mama katika kujifunza lugha ya pili yaani Kiswahili sanifu. Mathalani kubadilisha baadhi ya herufi na sauti za lugha ya Kiswahili. Kubadilisha sauti za Kiswahili ni athari kubwa katika lugha kwani ndizo zinazotofautisha maana. Pia sauti huunda silabi na silabi ndizo zinazounda maneno ya lugha mahususi. Kwahiyo, mtafiti alipochunguza Fonolojia ya lugha ya Kisukuma na Kiswahili amegundua kuwa lugha hizi mbili zinaingiliana pakubwa sana. Kuingiliana huku husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Athari hizi hutokea wakati mwanafunzi anapohamisha sauti aliyoizoea katika lugha yake ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine huchanganya matumizi ya sauti kwa sababu ya kuathirika na lugha ya kwanza. Wanafunzi hubabaika sana kwa sababu fonimu au sauti walizozizoea katika lugha ya Kisukuma hazipatikani katika lugha ya Kiswahili sanifu au zile zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hazipatikanani katika lugha ya Kisukuma. Data za utafiti huu zimebainisha athari zifuatazo za kifonolojia.

### 4.2.2 Athari za matumizi ya /l/ badala ya /r/

Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kwamba baadhi wa wazungumzaji wa lugha ya Kisukuma hutumia fonimu /l/ badala ya /r/. Hii ni dhahiri kuwa katika lugha ya Kisukuma wanatumia maneno mengi yanayoishia na herufi ya /l/ hivyo huchanganya

na herufi /r/ wanapozungumza Kiswahili sanifu. Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa kusoma dodoso za wanafunzi wanaozungumza lugha ya Kisukuma katika shule za msingi Mihayo, Kitete na Isike.

MFANO 1.

| **Lugha ya Kisukuma** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| Ngwala | Ngwara |
| Mpila | Mpira |
| Ipela | Pera |

Mifano hiyo hapo juu inaonesha jinsi wanafunzi wa Kiswahili sanifu ambao lugha yao ya kwanza ni Kisukuma wanavyotamka maneno ya Kiswahili yenye sauti /r/ kwa /l/. Ni dhahiri kwamba lugha ya Kisukuma ina herufi /l/ kwenye vitamkwa vya maneno yake mengi kwa sababu hii wanafunzi wengi wa jamii ya Kisukuma huchanganya wasijue jinsi ya kutumia fonimu hizi mbili ipasavyo. Wao hutumia fonimu /l/ mahali pa /r/ au /r/ badala ya /l/. Mwanafunzi anapojifunza Kiswahili inamlazimu kujifunza fonimu/ r/ isiyopatikana katika lugha yake ya kwanza. Mara nyingi wanafunzi wengi hukosa kutofautisha fonimu hizi mbili hii ni hutokana na athari za lugha ya kwanza. Matatizo hutokea wakati sauti aliyoizoea mwanafunzi katika lugha ya kwanza huwa haipatikani katika lugha ya Kiswahili sanifu. Hivyo mwanafunzi hutamka sauti iliyo karibu nayo. Katika mifano iliyoko hapo juu, mwanafunzi ametumia fonimu ya \l\ badala ya /r/.

### 4.2.3 Athari za matumizi ya /bh/

Fonimu /b/ ni kizuiwa (kipasuo) na ni sauti ya mdomo. Wakati wa kuitamka mdomo wa chini huelekeana na mdomo wa juu. Katika utamkaji wa sauti hii, mkondohewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu na kuzuiliwa kabisa mahali pa kuitamkia na kisha kuachiliwa ghafla. Sauti / b / hupotoshwa na kuwa / β / yaani silabi ba, be, bi, bo, bu hupotoshwa na kuwa bha, bhe, bhi, bho, bhu. Sauti / b / na /β/ zote ni sauti za midomo ingawa Sauti / b / ni kizuiwa, hutamkwa wakati mkondohewa unapofungiwa kabisa katika sehemu yoyote ya bomba la sauti na kisha kuruhusiwa upite ghafla. Na sauti /β/ ni kikwamizwa, hutamkwa wakati ala sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo. Kutokana na data za utafiti huu mtafiti amegundua kwamba, jamii ya Wasukuma wana herufi ya /bh/ katika lugha yao na huichanganya na fonimu za Kiswahili pindi wanapozungumza Lugha ya Kiswahili sanifu, Wanafunzi ambao ni wazumgumzaji wa Kisukuma hupachika fonimu ya /bh/ wanapozungumza fonimu ambayo haipatikani katika lugha ya Kiswahili sanifu, Hivyo wanafunzi hutumia sauti hii visivyo kwa sababu ya kuathiriwa na lugha ya kwanza. Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa kufanya mahojiano na wanafunzi wanaozungumza lugha ya Kisukuma katika shule za msingi Mayo, Kitete na Isike.

MFANO 2.

| Kisukuma | Kiswahili sanifu |
|---|---|
| Bhabha | Baba |
| Bhose | wote |
| Bhanhu | watu |

**Jedwali Na. 4.1: Athari za Kifonolojia Katika Matamshi kwa Wanafunzi wa shule za msingi**

| SHULE | Shule ya msingi Mihayo | | | Shule ya msingi Kitete | | | Shule ya msingi Isike | | | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Darasa | Darasa la 5 | Darasa la 6 | Darasa la 7 | Darasa la 5 | Darasa la 6 | Darasa la 7 | Darasa la 5 | Darasa la 6 | Darasa la 7 | | |
| Idadi ya wanafunzi | 1 | 2 | 3 | 1 | 2 | 3 | 1 | 2 | 3 | 18 | 100 |
| /I/ badala ya /r/ | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 08 | 44 |
| Matumizi ya /bh/ | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 04 | 22 |

FOMULA: $\mathbf{100} \times \frac{\text{watafitiwa}}{\text{Jumla kuu ya watafitiwa}} = \%$

**Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti.**

Jedwali hili linaonesha idadi ya wanafunzi walioathirika kimatumizi yaani kimatamshi katika shule hizo. Ambapo takribani kila darasa lina mwanafunzi mmoja hadi wanafunzi wawili, jedwali hili pia likionesha asilimia ya athari katika madarasa husika ya kijumuishwa. Kwa ujumla, katika sehemu hii mtafiti ameonesha baadhi ya maneno yaliyodhihirisha athari za kimatamshi katika lugha ya Kisukuma katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu. Aidha tumeeleza visababishi vya athari hizo, hutokana na tofauti mbalimbali za mifumo ya sauti na miundo ya maneno.

### 4.2.4 Athari katika matumizi ya / ð /

Fonimu hii ni kikwamizi na ni sauti ya meno, Hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondo hewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kwa kugusanisha alasogezi na alatuli kiasi kwamba sauti hutoka kwa kukwamakwama. Sauti / ð / hupotoshwa na kuwa / z

/ yaani silabi dha, dhe, dhi, dho, dhu hupotoshwa na kuwa za, ze, zi, zo, zu. Leonard (2001) anahusisha umuhimu wa mawasiliano ni kukuza uwezo wa kuwasiliana, lakini siyo kukuza ujuzi wa miundo au vipengele vya lugha tu, hivyo matamshi ni msingi muhimu sana katika mawasiliano, Hii ina maana kuwa unapojifunza lugha pia matamshi ya sauti lazima ujifunze ili katika mawasiliano pasiwepo na mgongano wa kutoelewana baina ya pande mbili. Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma walipokuwa wanajibu swali lililouliza **Je, kunatofauti gani kati ya kilimo cha sasa na cha zamani?** na Mtafitiwa A: alijibu

MFANO 3.

> **"Baazi ya wakulima tunatumia mfumo wa ulimaji wa kizamani"** na Mtafitiwa B: akasema, **"mimi nina zani kilimo cha sasa kinahitaji pesa nyingi tofauti na zamani"** Mtafiti aliweza kubaini athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: Mtafitiwa A alitamka neno **baazi** badala ya **baadhi** na mtafitiwa B alitamka neno **zani** badala ya **dhani**.

### 4.2.5 Athari katika matumizi ya / γ /

Fonimu hiyo ni kikwaruzo na ni sauti ya kaakaa laini (kaakaa la nyuma). Ni sauti ya nyuma kwani utamkaji wa sauti hii huambatana na sehemu ya nyuma ya ulimi, ambayo ni ala sogezi, kugusa kaakaa laini, ambalo ni ala sogezi pia, Hutamkwa wakati ala sauti zinapo karibiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida kiasi cha kusababisha mkwaruzo.

Sauti / γ / hupotoshwa na kuwa / g / yaani silabi gha, ghe, ghi, gho, ghu hupotoshwa na kuwa ga, ge, gi, go, gu. Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma walipokuwa wanajibu swali lililouliza, Kati ya sasa na zamani ni kipindi gani hasa umefurahia maisha? Nimambo gani yaliyokufanya ufurahie kipindi ulichofurahia na kuchukia kipindi ulichochukia? Mtafitiwa A: alisema

MFANO 4.

> Mtafitiwa A alisema: **"**Maisha ya siku hizi ni galama sana kwani vitu vingi tunanunua madukani tofauti na zamani tulikuwa tunavuna shambani" na mtafitiwa B: alisema "watu wengi sasa wanajenga nyumba nzuri za golofa ambazo ni nzuri tofauti na zamani maisha haya ya sasa yanamaendeleo mazuri" mtafitiwa C: alisema, "galama sasa inanifanya nisifurahie Maisha mazuri kwani mpaka kulima na kununua ng'ombe ni gali sana"**.** Mtafiti alibaini athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: Mtafitiwa A alitamka neno **galama** badala ya **gharama,** Mtafitiwa B alitamka neno **golofa** badala ya neno **ghorofa** na mtafitiwa C alitamka maneno **gali** badala ya **ghali** na **galama** badala ya **gharama**

### 4.2.6 Athari katika matumizi ya / ϴ /

Fonimu hii ni kikwamizi na ni sauti ya meno. Hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiweka katikati ya meno ya juu na ya chini. Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kwa kugusanisha alasogezi na

ala tuli kiasi kwamba sauti hutoka kwa kukwama kwama. Hii ni sauti ambayo katika utamkaji wake badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kwa kukwama kwama. Sauti / Ɵ / hupotoshwa na kuwa / s / yaani silabi tha, the, thi, tho, thu hupotoshwa na kuwa *sa, se, si, so, su.*

Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma walipokuwa wanajibu swali lililouliza Je, kunatofauti gani kati ya kilimo cha sasa na cha zamani? Mtafitiwa A: alisema

MFANO 5.

> “kilimo cha sasa **kinasamani** kubwa sana tofauti na miaka ile ya zamani kwa kuwa sasa tunapata pembejeo bora sana” mtafitiwa B: alisema “mfano mwaka jana nilipata magunia **selasini** ya tumbaku tofauti na kipindi cha nyuma nilikuwa napata magunia machache kama ishirini” Mtafiti aliweza kubaini athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: mtafitiwa A alitamka neno **samani** badala ya **thamani** aliposema na mtafitiwa B alitamka neno **selasini** badala ya **thelathini**.

Jedwali namba 42 linaonesha athari hizi za kifonolojia kitakwimu.

**Jedwali Na 4.2: Athari za Kifonolojia Katika Matamshi kwa wazee wa Kisukuma**

| Idadi ya wazee wa kisukuma | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|
| Wazee walioshiriki | 04 | 100 |
| Matumizi ya /z/ badal aya /dh/ | 02 | 40 |
| Matumizi ya /g/ badala ya /gh/ | 02 | 60 |
| Matumizi ya /s/ badal aya /th/ | 02 | 40 |

**FOMULA:** $100 \times \frac{\text{watafitiwa}}{\text{Jumla kuu ya watafitiwa}} = \%$

**Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti**

Athari za kifonolojia zilizobainika kwenye uchambuzi wa data ni matumizi ya /z/ badala ya /dh/, matumizi ya /g/badala ya /gh/. Matokeo haya yamejibu swali la kwanza la utafiti lililouliza, Kuna athari gani za kifonolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu? Aidha matokeo haya yamekamilisha lengo la kwanza la utafiti ambalo ni Kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

## 4.3 Athari za Kimofolojia

Lengo la pili la utafiti huu ni Kuchunguza athari za kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu. Data za utafiti huu zinathibitisha kuwa kuna athari za kimofolojia za lugha ya kisukuma ambazo pia zinajitokeza kwa wazungumzaji wa kisukuma wanaojifunza Kiswahili sanifu. Miongoni mwa athari zilizobainika ni kuongeza viambishi visivyohitajika katika maneno. Kwa mujibu wa Matinde (2012) viambishi ni vineno vilivyoshikishwa katika mzizi wa kitenzi kabla na hata baada ya mzizi wa kitenzi hicho.

### 4.3.1 Matumizi ya kiambishi ‘ga’

Baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kisukuma hupachika sauti ya \ga\ katika baadhi ya maneno kwa lengo la kuonesha hali ya mazoea na kisha kupata miundo isiyo sahihi. Mifano hiyo hapo chini inadhihirisha athari za kimatumizi ya maneno zilizojibainisha wakati wa kusoma dodoso za wanafunzi wanaozungumza lugha ya Kisukuma katika shule za msingi Mihayo, Kitete na Isike.

Utafiti huu umebaini matumizi ya kiambishi ‘ga’ katika maneno mengi ya Kiswahili ambacho hutumika kuonesha hali ya mazoea. Mifano ifuatayo inathibitisha matumizi ya kiambishi hiki kwenye Kiswahili sanifu; Katika sarufi ya Kiswahili hakuna kiambishi cha aina hii kinachoonesha hali ya mazoea, badala yake ni kiambishi ‘hu’ ndicho hufanya kazi hiyo.

MFANO 5.

| Kiswahili sanifu | Kiswahili cha wasukuma |
|---|---|
| Oa | oaga |
| Soma | somaga |
| Chagua | chaguaga |

Kwa kuongeza, watafitiwa ambao ni walimu wa somo la Kiswahili walijibu swali lililouliza je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza Lugha ya Kiswahili sawa sawa? Mtafitiwa A: alijibu

MFANO 6.

> **“**Wanafunzi wetu wanatabia siyo tu ya kuongea bali hata kuandika maneno ya kuongeza ambayo si sanifu**”** na mtafitiwa B: alijibu “utamsikia mwalimu au mwanafunzi akizungumza anasema, napendaga badala ya huwanapenda”.

**Jedwali Na. 4.3 Jedwali la watafitiwa walimu linalo onesha idadi na majibu yao.**

| Idadi ya walimu walioshiriki | Jumla | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|---|
| Walioshiriki | 8 | | |
| Je wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza lugha ya Kiswahili sawa sawa? | | 06 | 02 |

**Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti**

Kama inavyooneshwa katika jedwali hapo juu, walimu wa lugha ya Kiswahili waliotafitiwa wote 10 ambao ni sawa na 100 walijibu NDIYO ambao walikuwa 06 katika swali Je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza lugha ya Kiswahili sawa sawa? Ambao ni sawa sawa na asilimia 60 na waliojibu HAPANA ambao ni sawa sawa na asilimia

40. Utafiti huu umebaini kuwa katika lugha ya Kisukuma, fonimu /ga/ hutumika kama kimalizikio cha maneno mengi hali hii inasababisha wengi kutamka maneno yenye sauti hii kwa kupachika fonimu hii pasipostahili hasa miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu huchanganyikiwa na kukosa kujua waitumie sauti hiyo wapi.

### 4.3.2 Matumizi ya kiambishi ‘gi’

Data za utafiti pia zimeonesha kiambishi ‘gi’ kikitumika katika baadhi ya maneno ya Kiswahili kuonesha hali ya ukanushi. Mifano ifuatayo inathibitisha matumizi ya kiambishi hiki kwenye Kiswahili sanifu; Katika sarufi ya Kiswahili hakuna kiambishi cha aina hii kinachoonesha hali ya ukanushi.

| Kiswahili sanifu | Wasukuma |
|---|---|
| sili | silagi |
| silali | silalagi |

Kwa kuongeza, watafitiwa ambao ni walimu wa somo la Kiswahili walijibu swali lililouliza je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza Lugha ya Kiswahili sawa sawa?

MFANO 7.

Mtafitiwa A: alijibu "Utamsikia mwalimu au mwanafunzi akizungumza anasema, s**ilagi** badala ya **huwasili**" pia watafitiwa wengine ambao ni walimu wa somo la Kiswahili walijibu maswali mengine yaliyouliza, Nieleze mbinu mbalimbali mnazotumia hapa shuleni kuwahamasisha wanafunzi kufaulu somo la Kiswahili? Mtafitiwa B: alijibu "shuleni hapa tunatumia michezo kama ngoma, ngonjera, pia midahalo ambayo huwaleta pamoja wanafunzi wanaojifunza somo la Kiswahili na huwafanya kushindana katika ngonjera, kucheza ngoma pamoja na kushiriki midahalo" mtafitiwa mwingine alijibu swali Kama utapewa nafasi ya kuishauri serikali kuhusu sera ya lugha na elimu utaishauri nini? Mtafitiwa C: alisema "katika ufundishaji wetu kunatatizo kubwa la kila mwalimu kufundisha somo zaidi ya moja na hii hufanya walimu wasiokuwa mahiri katika somo husika la Kiswahili husababisha makosa ya ufundishaji kama vile utamkaji mzuri, hivyo ni vyema serikali iweke mgawanyo wa walimu kufundisha somo moja au mawili wanayo ya mudu."

Kwa ujumla utafiti huu ulibaini kuwa Wasukuma wengi huongeza vitamkwa visivyo vya lazima katika maneno ya lugha ya Kiswahili. Aidha katika Kiswahili sanifu viambishi tamati hivi havipo kamwe lakini wazungumzaji wa Kisukuma wanaojifunza Kiswahili sanifu huvitumia kwa sababu mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu anaposikia utamkaji wa maneno ya Kiswahili kwa namna hii hujua moja kwa moja kuwa anayezungumza si mahiri katika lugha ya Kiswahili. Hizo ni athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Athari hizo hudhihirika pale mzungumzaji anapotamka sauti ya Kiswahili maana hutumia matamishi na lafudhi ya lugha ya Kisukuma. Mzungumzaji wa Lugha ya Kisukuma hutumia nguvu sana wakati wa kutamka maneno hivyo hivyo wakati wa kuzungumza Lugha ya Kiswahili hutumia nguvu ile ile, ndiyo maana wanaongea maneno kwa kuweka mkazo hata pasipohitajika.

Kutokana na mifano hiyo hapo juu, ni dhahiri kwamba lugha ya Kisukuma huathiri pakubwa lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji, pia wanafunzi hutatizwa na lugha kwa sababu ya matamshi ya sauti walizozoea katika lugha ya kwanza hazipatikani katika lugha ya pili. Athari hizi hutokea kwa sababu ya tofauti iliyopo ya matamshi ya sauti baina ya lugha hizi mbili. Kutokana na kutofautiana kwa matamshi ya sauti na kimuundo katika baadhi ya maneno pamoja na matamshi mabaya ya mwalimu wakati wa ufundishaji wa wanafunzi wa Kisukuma.

### 4.4 Viwango vya utokeaji wa athari za kifonolojia, na kimofolojia za lugha yaKisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu

Lengo la tatu la utafiti huu ni kutathmini kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia, na kimofolojia ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya

Kiswahili sanifu. Data za utafitihuu zinathibitisha utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia kwa wazungumzaji wa lugha ya Kisukuma wanaojifunza Kiswahili sanifu. Mtafiti alichunguza athari za kifonolojia na kimofolojia kwa wasemaji wa Kisukuma wanaojifunza Kiswahili kupitia uchambuzi wa madodoso aliyowapatia watafitiwa, katika maswali mbalimbali yaliyoulizwa na mtafiti kwa watafitiwa yaliweza kuonesha viwango vya athari kama vile katika kipengele cha kifonolojia athari mbalimbali zilibainika kupitia majibu ya watafitiwa mfano katika majibu ya maswali yaliyoulizwa Je, kuna tofauti gani kati ya kilimo cha sasa na cha zamani? na Mtafitiwa A: alijibu

MFANO 8.

"baazi ya wakulima tunatumia mfumo wa ulimaji wa kizamani" na Mtafitiwa B: akasema, "mimi nina zani kilimo cha sasa kinahitaji pesa nyingi tofauti na zamani" Mtafiti aliweza kubaini athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: Mtafitiwa A alitamka neno baazi badala ya baadhi na mtafitiwa B alitamka neno zani badala ya dhani. Swali lingine lililobainisha athari kifonolojia Kati ya sasa na zamani ni kipindi gani hasa umefurahia maisha? Nimambo gani yaliyokufanya ufurahie kipindi ulichofurahia na kuchukia kipindi ulichochukia? Mtafitiwa A: alisema"Maisha ya siku hizi ni galama sana kwani vitu vingi tunanunua madukani tofauti na zamani tulikuwa tunavuna shambani" na mtafitiwa B: alisema "watu wengi sasa wanajenga nyumba nzuri za golofa ambazo ni nzuri tofauti na zamani maisha haya ya sasa yanamaendeleo mazuri" mtafitiwa C: alisema, "galama sasa inanifanya nisifurahie Maisha mazuri kwani mpaka kulima na kununua ng'ombe ni gali sana" Mtafiti aliweza kubaini

athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: Mtafitiwa A alitamka neno galama badala ya gharama, Mtafitiwa B alitamka neno golofa badala ya neno ghorofa na mtafitiwa C alitamka maneno gali badala ya ghali na galama badala ya gharama, Swali lingine lililobainisha kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia ni, Je, kunatofauti gani kati ya kilimo cha sasa na cha zamani? Mtafitiwa A: alisema "kilimo cha sasa kinasamani kubwa sana tofauti na miaka ile ya zamani kwa kuwa sasa tunapata pembejeo bora sana" mtafitiwa B: alisema "mfano mwaka jana nilipata magunia selasini ya tumbaku tofauti na kipindi cha nyuma nilikuwa napata magunia machache kama ishirini" Mtafiti aliweza kubaini athari za matumizi ya maneno wakati wa mahojiano na wamilisi wa lugha ya Kisukuma kama ifuatavyo: mtafitiwa A alitamka neno samani badala ya thamani aliposema na mtafitiwa B alitamka neno selasini badala ya thelathini. Katika uchambuzi wa data za utafiti mtafiti amebaini katika athari za kifonolojia viwango vya athari zilikuwa na asilimia zifuatazo:

**Jedwali Na. 4.4 La watafitiwa linalo onesha idadi ya kiwango cha athari za kifonolojia katika Kiswahili sanifu.**

| Athari za kifonolojia | Kiwango cha athari |
|---|---|
| Matumizi ya /I/ badal aya /r/ | 44% |
| Matumizi ya bh/ badal aya /b/ | 22% |
| Matumizi ya /z/ badal aya /dh/ | 40% |
| Matumizi ya /g/ badal aya /gh/ | 60% |
| Matumizi ya /s/ badal aya /th/ | 40% |

FOMULA: $100 \times \frac{\text{watafitiwa}}{\text{Jumla kuu ya watafitiwa}} = \%$

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti.

Pia katika kipengele cha kimofolojia athari mbalimbali zilibainika kupitia majibu ya watafitiwa mfano katika majibu ya maswali yaliyoulizwa na mtafiti kwa watafitiwa, je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza Lugha ya Kiswahili sawa sawa? Mtafitiwa A: alijibu

MFANO 9.

> "Wanafunzi wetu wanatabia siyo tu ya kuongea bali hata kuandika maneno ya kuongeza ambayo si sanifu" na mtafitiwa B: alijibu "utamsikia mwalimu au mwanafunzi akizungumza anasema, napendaga badala ya huwanapenda" Kwa kuongeza, watafitiwa ambao ni walimu wa somo la Kiswahili walijibu swali lililouliza je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza Lugha ya Kiswahili sawa sawa? Mtafitiwa A: alijibu "utamsikia mwalimu au mwanafunzi akizungumza anasema, silagi badala ya huwasili" Katika uchambuzi wa data za utafiti mtafiti amebaini katika athari za kimofolojia viwango vya athari zilikuwa na asilimia zifuatazo:

**Jedwali Na 4.5 La watatitiwa i linalo onesha idadi ya kiwango cha athari za kimofolojia katika Kiswahili sanifu**

| Athari za kimofolojia | Kiwango cha athari |
|---|---|
| Athari ya /ga/ | 60% |
| Athari ya /gi/ | 10% |

**FOMULA:** $100 \times \frac{\text{watafitiwa}}{\text{Jumla kuu ya watafitiwa}} = \%$

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti.

Athari kubwa za kifonolojia na kimofolojia alizogundua mtafiti, ilihusisha matamshi, kuongeza viambishi ambavyo vilitokana katika lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Imejitokeza wazi kuwa lugha ya Kisukuma imeathiri lugha ya Kiswahili na hivyo kusababisha makosa ya aina mbalimbali. Kiwango kikubwa cha athari alichokipata mtafiti baada ya kuwatafiti watafitiwa mbalimbali alibaini kwamba kiwango cha kifonolojia kimeleta athari kubwa kuliko kimofolojia.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imefanikiwa kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo mahususi ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti yameweza kubainisha sifa athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza Kiswahili kwa kurejelea vipengele vya kifonolojia na kimofolojia.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekeo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni mapendekezo na sehemu ya tatu ni hitimisho la utafiti huu.

### 5.2 Muhtasari kwa ujumla wa Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa shule za msingi. Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu. Kwanza kuchunguza athari za kifonolojia ya lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Pili, kuchunguza athari za kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Tatu, kutathmini kiwango cha utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kisukuma katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo: Kuna athari gani za kifonolojia za Lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu? Kuna athari gani za kimofolojia za Lugha ya Kisukuma katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu? Na swali la tatu, kuna viwango vipi vya utokeaji wa athari za kifonolojia na kimofolojia ya Lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu? Utafiti huu ulifanyika katika Mkoa wa Tabora katika wilaya ya Tabora mjini. Ulichunguza maoni, mitazamo na uelewa wa walimu, na wanafunzi na wazungumzaji hasa wanaofahamu lugha ya Kisukuma na Kiswahili. Nia kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza athari za

lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa shule za msingi. Utafiti huu ulitumia watafitiwa 44 waliotumika kama sampuli ya utafiti huu. Watafitiwa walikuwa wanafunzi wa darasa la 5, 6 na 7 na walimu katika shule ya msingi Isike, Mwenge, Mihayo na shule ya msingi Kitete. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu ni hojaji na mahojiano.

## 5.3 Muhtasari wa matokeo

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa kuna tofauti kubwa ya mfumo wa kifonolojia na kimofolojia wa lugha ya Kisukuma na Kiswahili ambayo huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wazungumzaji wa Kisukuma. Aidha mtafiti ameweza kubaini athari za matamshi kwa uchopekaji, udondoshaji, uongezaji wa viambishi. Vile vile, mtafiti ameweza kuthibitisha kuwa athari hizo, husababishwa na wazungumzaji kuchanganya mpangilio wa lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti huu pia umebaini kuwa kati ya makosa ya kifonolojia na kimofolojia, makosa yanayotokea kwa wingi kwa wazungumzaji wa Kisukuma wanaojifunza Kiswahili ni makosa ya kifonolojia.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulikusudia kutathmini athari za lugha ya kisukuma katika kujifunza Kiswahili sanifu, utafiti huu umebainisha kwamba zipo athari mbalimbali zinazofanywa naa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii hii kama vile, dosari za udondoshaji wa viambishi na upachikaji wa viambishi. Pamoja na dosari hizo, imebainika pia kwamba zipo sababu kadhaa zinazosababisha dosari hizo na kumfanya mjifunzaji ashindwe kufikia umilisi wa mzawa wa lugha hiyo. Sababu hizo ni kama vile: athari za lugha ya kwanza mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya

pili, tofauti za kimuundo kati ya lugha ya Kiswahili na Kisukuma, walimu kutokuwa na maarifa kamili ya lugha wanayoifundisha na kutokuwa na ujuzi wa kuifundisha na uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti anapendkeza maeneo mengine yanayohusiana na utafiti huu yaweze kushughulikiwa na watafiti wegine. Kwanza, utafiti huu umeshughulikia athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu, mtafiti anapendekeza watafiti wengine wafanye utafiti juu ya athari za lugha nyingine za Kibantuzinazotokana na tofauti za kisarufi baina ya lugha lugha za Kibantu na Kiswahili. Pili, wazazi waelimishwe juu ya umuhimu wa kutumia Lugha ya Kiswahili ili waone umuhimu wa kuwa wanazungumza na kuwasiliana na watoto wao kwa kutumia Lugha ya Kiswahili. Tatu, uchnguzi mwingine ufanyike wa mbinu za ufundishaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

## MAREJELEO

Berg, B.C. (2007). *Qualitative Research methods for the social sciences,* (6th Ed) Calfornia:Person Education Inc

Chaochuan, Y. (2005). Second Language Learning: Conscious or Unconscious? CELEA 28(4): 24-31.

Ellis, R. (1985). Understanding Second Language Acquisition. Oxford: Oxford University Press.

Jackendoff, R. (1994). Patterns in the Mind: Language and Human Nature. New York: Basic.

Kombo, D. & Tromp, A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *An Introduction.* Nairobi:Paulines Publications Africa.

Kothari, R. (2008). *Research Methodology*. New Delhi: New Age International Publishing (T).

Kothari, R. (2004). Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi: New Age publishers.

Kress, T. M. (2008). Critical Praxis Research; Breathing New Life into Research Methods for Teachers. United States of America: Springer

Lado, R. (1957). Linguistics Across Cultures: Applied Linguistics for Language Teachers. Ann Arbor: University of Michigan Press.

Lenneberg, E. (1967). Biological Foundations of Language. New York: Wiley.

Massamba, D. (2004), Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha, Dar es Salaam: TUKI

Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya lugha, Isimu na Nadharia*, *Kwa Sekondari, vyuo vya kati na vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Education publishers (T) LTD.

Mayala, M.B. (1971). *Sukuma Expression of Traditional Religion in Life*. EastAfrica.

McNamara, T. (2000). Language Testing. Hong Kong: Oxford University press.

Mdee, S, J. (2011). Kamusi ya Karne ya 21; Kamusi ya Kiswahili yenye Uketo zaidi katika Karne Hii. Nairobi: Longman Publisher LTD.

Mekacha, R. (2011). Isimu jamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili. Dar es Salaam: TATAKI.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu*, *Fonetiki*, *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn publishers.

Mgullu, R.S. (2011). Mtaala wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn Publishers

Mlingo, E.S. (2012). Jifunze utafiti. Mwongozo kuhusu utafiti na utamaduni wa ripoti yenye mantiki. Ecumerical Gathering (EGY): Dar es Salam.

Muungwana blog (2017) http://www.muungwana.co.tz/2017/05/haya-ndio-makabila-125-ya-tanzania.html.

Nyanda, J. (2015). Athari za Lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Lugha ya Kiswahili, Tasnifu ya Kiswahili The Open University of Tanzania.

O'Grady, W. (2008). How Children Learn Language. Fifth edition. Cambridge: Cambridge University Press.

Riro, S.M. (2012) Dafina ya lugha isimu na nadharia: kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, Mwanza, Tanzania: Serengeti educational publishers (T) LTD.

Saville-Troike, M. (2006). Introducing Second Language Acquisition. New York: Cambridge University Press.

Spolsky, B. (1989). Conditions for second language learning. Oxford: Oxford University Press.

Stern, H. H. (1983). Fundamental Concepts of Language Teaching. Oxford: Oxford University Press.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*; TUKI: Dar Es Salaam

UNESCO. (2003). Education in a Multilingual World. Paris UNESCO (UNESCO EducationPositionPaper). http://unesdoc.unesco.org/images/0012/001297/129728e.pdf.1Accessed 25th September 2018

Walliman, N. (2011). Research Methods; The Basic. London & New York: Routledge Taylor &Francis Group

Wamitila. (2003). Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Weinreich, U. (1953). Languages in Contact. The Hague: Mouton.

Wenceslaus, M. (2015). Athari za Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri : The Open University of Tanzania.

# VIAMBATANISHO

## KIANBATANISHO NA 01

MASWALI YA HOJAJI (DODOSO) KWA WANAFUNZI WAKISUKUMA WA SHULEZA MSINGI WANAOJIFUNZA SOMO LA KISWAHILI.

Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.Ninafanya Utafiti juu ya Athari za Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu. Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya Shahada ya Uzamili. Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilishautafiti huu. Toa habari za kweli bila woga wowote. Usiandike jina lako. Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu. Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

Umri......................................

Jinsi.....................................

Darasa la...................................

Badilisha sentensi zifuatazo kutoka katika lugha ya Kisukuma kwenda Kiswahili

1. Natogirwe kosoma gitabo
2. Ng’wana alelela sana
3. Mayuu akulimaga kungunda
4. Bhabha alebhina mbina
5. Nalelomba minze ga kongwa
6. Nalogoha mihayo ying’we
7. Mayo shilewa shelyaga?

8. Ng'wanone wasayaga
9. Shilewa sha ngoko sheshilaga
10. Aleyo etuja jeneji jikoshila nanale?
11. Mihayo minje natahayile
12. Ndwala ingelaga mchalo
13. Ntondobonge nadogijipandeka logendo
14. Mami wanitanile kaya
15. Magongoli minge nho eng'wakono
16. Mbula eletoka bolegwa
17. Nakokolwa mpaga nanale?
18. Masala kolangwa
19. Nakombolaga kaya
20. Sebha akojiwe
21. Shilewa sha lelo shanilemelaga gete
22. Mashenho gange gakogohe
23. Mva ya habhise nyobha
24. Gilongaga mayanga omunzengo gwise
25. Ntondo nakuze kokoyelela
26. Mulungu ntale pye ikoshila
27. Nilombelage bhopanga duhu

**KIAMBATANISHO NA 02**

MASWALI YA MAHOJIANO KWA WALIMU WAFUNDISHAO SOMO LA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA MSINGI

Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya Utafiti juu ya Athari za Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu. Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya Shahada ya Uzamili. Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilishautafiti huu. Toa habari za kweli bila woga wowote. Usiandike jina lako. Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu. Ninatanguliza shukurani za dhatikwa ushirikiano wako.

Umri..............................................................................................

Jinsi..............................................................................................

Kiwango cha elimu......................................................................

1) Je, wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa wanazungumza lugha ya Kiswahili sawa sawa?

2) Vipi kuhusu kiwango cha ufaulu wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa?

3) Wewe ukiwa ni mwalimu wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kisukuma shuleni hapa;

   a) Nieleze mbinu mbalimbali mnazotumia hapa shuleni kuwahamasisha wanafunzi kufaulusomo la Kiswahili.

   b). Kama utapewa nafasi ya kuishauri serikali kuhusu sera ya lugha na elimu utaishauri nini?

# KIAMBATANISHO NA 03

**The United Republic of Tanzania**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Telegrams: **MKUUMKOA**
Telephone: 026 2604058/2604116
Fax: 026 – 2604274
Email: ras.tabora@tamisemi.go.tz
In reply please quotes

Ref No DA. 116/247/01/237

Regional Commission's Office,
P.O.Box. 25,
**TABORA.**

29th Julai, 2020.

Municipal Director
**TABORA MC**

**REF: REQUEST FOR RESEARCH CLEARANCE.**

Please refer to the heading above.

We received letter from OpenUniversity of Tanzania with Ref.PG201705223 of date 25th Juni 2020 introducing Mr.Paschal.M. Mulikuza and ask to grant permission to collect data on research proposal " **Kuchunguza athari za lugha ya kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu"** I would like to Inform that the permission is offered to collect data for the period from 1st Julai to 27th August, 2020. For this letter I kindly request your office to grant him any assistant to accomplish their research requirement for partial fulfilment of the requirement for the completion of his study.

Yours sincerely,

**RUKIA S. MANDUTA**
FOR: REGIONAL ADMINISTRATIVE SECRETARY
**TABORA**

Copy: Regional Administrative Secretary (**To see in the file**)
**TABORA.**

Districtic Admistrative Secretary
**Tabora** (For Information)

Vice Chancellor
The Open University Of Tanzania (*Instructed to submit research*
**P.O. Box 23409** *finding , Collected information for this permit is not*
**Dar Es Salaam** *for publication*)

✓ Mr. Pascal. M. Mulikuza (For identification)
**Student.**